KHGIVF

# PROGRAMU YA UPANDIKIZAJI WA MIMBA



Maswali Yaulizwayo Kila Mara

**Ugumba ni nini?**

Ni kutokuwa na uwezo wa kupata mimba baada ya mwaka mmoja mpaka miwili wa kujaribu kupata mimba kwa kujamiiana bila kinga.

**Je, ni sababu gani ambazo husababisha ugumba?**

• Kwa wanawake ni umri, matatizo ya kutengeneza mayai, kuziba au kuharibika kwa mirija ya uzazi, matatizo katika mfuko wa uzazi kama vile uwepo wa uvimbe kwenye mfuko wa uzazi na endometriosisi (changamoto ya tishu kuwa nje ya mfuko wa kikazi ambazo zinapaswa kuwa ndani).

• Kwa wanaume ni uwezo mdogo wa kasi ya mbegu za kiume, kushindwa kutengeneza mbegu za kutosha, kuziba kwa njia za uzazi, na shahawa zisizo za kawaida.



**Ni wakati gani ninapaswa kutembelea kliniki wakati wa mzunguko wangu wa hedhi?**

- Kwa wagonjwa wa mara ya kwanza, tunapendekeza utembelee kliniki siku ya 10 ya mzunguko wako wa hedhi.
- Wagonjwa wanaopanga kuanzisha mpango wa IVF / ICSI wanashauriwa kuja siku ya 2 ya mzunguko wa hedhi.

**Je *intrauterine insemination (IUI)* ni nini?**

**IUI** ndiyo njia rahisi zaidi ya matibabu inayopatikana kwa wanandoa au wenza wasio na uwezo wa kuzaa na




inahusisha kuchomwa sindano yenye sampuli ya mbegu za kiume zilizo bora kwenye mfuko wa uzazi wa wanawake.

**Je *in-vitro fertilization (IVF)* ni nini?**

**IVF** ni utaratibu unaohusisha ukusanyaji wa mayai kutoka kwenye ovari, kurutubisha mayai kwenye maabara kwa kutumia mbegu za kiume, kukuza viinitete kwa siku chache na kuhamisha baadhi ya viinitete kwenda katika mfuko wa uzazi kwa ajili ya kupandikizwa kwa mimba.

- IVF hufahamika pia kama ***"test-tube baby".***

**Je *intracytoplasmic sperm injection (ICSI)* ni nini?**

**ICSI** ni utaratibu unaohusisha kuchomwa sindano yenye mbegu za kiume kwenye kila yai lililokomaa ili kuruhusu utungwaji wa mimba kutokea.

**Je *preimplantation genetic screening (PGS)* ni nini?**

**PGS** ni utaratibu ambao hauangalii upungufu fulani maalum bali hujikita katika kuangalia na kuzitathimini kromosomu zenye mapungufu katika kromosomu 23 kwenye kiinitete.

**Nani anapaswa kufanyiwa matibabu ya IUI, IVF, ICSI au PGS?**

**IUI** - Matatibabu haya yatafanyika kwa wanawake walio na mirija ya kawaida ya uzazi na ambao wana Waume wenye idadi ya mbegu za kiume ya kawaida au iliyopungua kidogo.

**IVF** - Matatibabu haya yatafanyika kwa wanawake walio na mirija ya uzazi iliyoharibika na isiyoweza kutibika, iliyoziba au walio na endometriosisi, wenye changamoto ya utendaji kazi wa ovari, ugumba usioelezeka na tatizo la kinga ya mwili. Pia Wanawake hawa wana Waume wenye idadi ya kawaida ya mbegu za kiume au idadi iliyo bora zaidi.

**ICSI** - Matatibabu haya yatafanyika kwa Wanawake walio na umri wa zaidi ya miaka 39 au Waume walio na mbegu zenye ubora duni, mbegu zilizoganda, mbegu zilizotolewa kutoka kwa tishu za korodani au ambao wana historia ya kuwa ya kiwango kidogo cha uwezo wa kutungisha mimba katika mizunguko iliyopita.

**PGS** - Matatibabu haya yatafanyika kwa Wanawake walio na umri mkubwa wa uzazi, ambao mimba nyingi zimeshaharibika na ambao zoezi la uhamishaji wa kiinitete kwenda kwenye mfuko wa uzazi limefeli mara kadhaa.

**Je, mume wangu anapaswa kuwepo katika miadi yangu yote ya matibabu?**

- Hapana siyo yote. Hata hivyo, mume wako atatakiwa kuja katika miadi hii ifuatayo:

a) Uchunguzi wa ubora wa mbegu zake kabla ya mpango wa IVF au ICSI.
b) Kikao cha awali cha ushauri.
c) Siku ya kurejesha yai na uhamisho wa kiinitete.



**Je, mume wangu anaweza kukusanya mbegu zake akiwa nyumbani?**

Ndiyo, Lakini atapaswa kufuata ushauri sahihi kutoka kwa wataalamu wetu.

**Je, ni madhara gani ya dawa za upandikizaji mimba ambayo hutokea mara kadhaa?**

- Ni kawaida kuhisi tumbo limejaa, kuwa na mihemuko au kuhisi joto kali.
- Matibabu yanaweza kuleta athari za ngozi katika eneo ulilochomwa sindano ya upandikizaji.
- Asilimia ndogo ya wagonjwa wanaweza kupata changamoto ya hyperstimulation (Hali inayotokana na kuzidi kwa kiasi cha homoni wakati wa matibabu)

**Je kwa wastani, ni idadi gani ya viinitete inayohamishwa?**

Kwa ujumla, viini viwili au vitatu vitahamishwa baada ya majadiliano na daktari.

**Je, ni nini kitafanyika kwa viinitete vyangu vitakavyobakia?**

Wakati wote tunawashauri wagonjwa wetu juu ya kugandisha na kuhifadhi viinitete vyao vilivyobakia kwenye maabara yetu kwa matumizi yao ya baadaye.

**Je, ni wakati gani unaofaa kuanza mzunguko mpya wa IVF baada ya mzunguko wa awali ambao haujafanikiwa?**

- Unaweza kujaribu tena baada ya mapumziko ya miezi 2 hadi 3
- Ikiwa una viinitete vilivyogandishwa, daktari wetu atakuandaa na kutekeleza uhamisho wa viinitete vilivyo gandishwa chini ya uangalizi maalum.

**Je, kuna ukomo wa umri ili kufanikisha programu ya IVF?**

- Hakuna kikomo cha umri lakini hatuwashauri wanawake wenye umri zaidi ya miaka 50 kufanya matibabu haya.
- Uwezekano wa kupata mimba hupungua kadri umri unavyosonga.

**Je, mzunguko wa IVF huchukua muda gani?**

- Inachukua muda wa mwezi mmoja na nusu ili kukamilisha mzunguko wa IVF.
- Hii inajumuisha udhibiti wa homoni, sindano za kuchochea uzalishaji wa mayai na utaratibu kamili wa maabara ya IVF.

KHGIVF

# Mawasiliano

**Kairuki Hospital Green IVF**
Bunju A Mianzini, Dar es Salaam,
Tanzania 14125
Simu: +255 757 414 918
Barua Pepe: info@kairukiivf.org
Website: www.kairukiivf.org

